# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 1001

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Fasihi ya Kiswahili Elimu ya Sekondari Kidato cha III - IV

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-785-2

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Fasihi ya Kiswahili Elimu ya Sekondari Kidato cha III - IV nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA FASIHI YA KISWAHILI ELIMU YA SEKONDARI

## KIDATO CHA III–IV

## 2023

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2023

Toleo la kwanza, 2023

ISBN: 978-9987-09-785-2

Taasisi ya Elimu Tanzania

S. L. P. 35094

Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255-735041168 / +255-735041170

Baruapepe: director.general@tie.go.tz

Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (2023). *Muhtasari wa Fasihi ya Kiswahili Elimu ya Sekondari Kidato cha III–IV*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

# Yaliyomo


Orodha ya Majedwali ........ iv
Vifupisho ........ v
Shukurani ........ vi
1.0 Utangulizi ........ 1
2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania ........ 1
3.0 Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV ........ 2
4.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV ........ 3
5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi ........ 3
6.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 4
6.1 Mwalimu ........ 4
6.2 Mwanafunzi ........ 5
6.3 Mzazi/Mlezi ........ 5
7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 6
8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 6
9.0 Upimaji ........ 6
10.0 Idadi ya Vipindi ........ 7
11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 7
Bibliografia ........ 35





FASIHI YA KISWAHILISEKONDARI KIDATO CHA III-IV.indd 3 08/08/2023 15:07

# Orodha ya Majedwali


Jedwali Na. 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Kidato cha III–IV ........ 3

Jedwali Na. 2: Mgawanyo  wa Alama za Upimaji Endelevu na Tamati ........ 7

Jedwali Na. 3: Maudhui ya Kidato cha III ........ 8

Jedwali Na. 4: Maudhui ya Kidato cha IV ........ 23

## Vifupisho

| | |
|---|---|
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |



FASIHI YA KISWAHILISEKONDARI KIDATO CHA III-IV.indd 5 08/08/2023 15:07

# Shukurani

Maandalizi ya Muhtasari wa Fasihi ya Kiswahili Elimu ya Sekondari Kidato cha III–IV yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zisizo za serikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha uandaaji wa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu, pamoja na wakuza mitaala wa TET. Vilevile, TET inaishukuru kwa dhati Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwa na wahitimu wenye maarifa, ujuzi na mwelekeo utakaowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndilo lengo kuu la Uboreshaji wa Mitaala ya Elimu ya Mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.



Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
**Taasisi ya Elimu Tanzania**



FASIHI YA KISWAHILISEKONDARI KIDATO CHA III-IV.indd 6 08/08/2023 15:07

## 1.0 Utangulizi

Somo la Fasihi ya Kiswahili ni moja kati ya masomo chaguzi katika Elimu ya Sekondari Kidato cha III–IV kwa wanafunzi walioko katika Mkondo wa Elimu ya Jumla. Lengo la kujifunza somo la Fasihi ya Kiswahili ni kumjengea mwanafunzi maarifa, stadi na mwelekeo utakaomwezesha kuthamini kazi za fasihi ya Kiswahili na kujenga ujumi na falsafa ya Kiafrika katika kazi za fasihi. Vilevile, mwanafunzi ataweza kutathmini mbinu za kisanaa za utunzi wa kazi za kifasihi na kuzitumia katika kubuni kazi za fasihi pamoja na kutambua fursa zitakazomwezesha kujiajiri au kuajiriwa.

Muhtasari huu umeandaliwa ili kuongoza ufundishaji na ujifunzaji wa Fasihi ya Kiswahili Elimu ya Sekondari Kidato cha III–IV katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, muhtasari huu unatafsiri umahiri uliobainishwa kwenye Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV wa Mwaka 2023. Pia, Muhtasari unatoa maelekezo ya kumwezesha mwalimu kuandaa mchakato wa ufundishaji kwa ufanisi. Vilevile, muhtasari unatoa nafasi inayomwezesha mwalimu kutumia mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Fasihi ya Kiswahili zitakazokuza stadi za karne ya 21 zikiwemo ubunifu, mawasiliano, ushirikiano, fikra tunduizi na utatuzi wa changamoto.

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu nchini Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;

(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;

(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;

(d) Kuelewa na kulinda tunu za taifa, ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya taifa;

(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;

(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;



FASIHI YA KISWAHILISEKONDARI KIDATO CHA III-IV.indd 1 08/08/2023 15:07

(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na

(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV

Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV Elimu ya Jumla ni:

(a) Kuimarisha, kupanua na kuendeleza uelewa wa kina wa maarifa, stadi na mwelekeo alioupata katika hatua ya elimu ya msingi;

(b) Kulinda mila na desturi, umoja wa kitaifa, tunu za taifa, demokrasia, kuthamini haki za binadamu na za kiraia, wajibu na majukumu yanayoendana na haki hizo;

(c) Kukuza tabia ya kujiamini na uwezo wa kujifunza kwenye nyanja mbalimbali zikiwemo sayansi na teknolojia, maarifa ya kinadharia, na kiufundi;

(d) Kuimarisha mawasiliano kwa kutumia stadi za lugha ikiwemo Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT), lugha mguso, lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Aidha, mwanafunzi ahamasishwe kumudu angalau lugha moja nyingine ya kigeni kulingana na hali halisi ya shule yake;

(e) Kuimarisha uwajibikaji katika masuala mtambuka ya kijamii yakiwemo afya, usalama, usawa wa kijinsia na utunzaji endelevu wa mazingira;

(f) Kujenga ujuzi na stadi mbalimbali zitakazomwezesha kujiajiri, kuajiriwa, na kuyamudu maisha kwa kutumia vizuri mazingira yake; na

(g) Kukuza utayari wa kujiendeleza na mafunzo ya elimu ya kati na ya juu.



FASIHI YA KISWAHILISEKONDARI KIDATO CHA III-IV.indd 2 08/08/2023 15:07

## 4.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV

Umahiri wa jumla wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV Elimu ya Jumla ni:

(a) Kutumia maarifa na stadi alizozipata katika ngazi ya elimu ya msingi kuimarisha na kupanua uelewa wa kitaaluma;
(b) Kuthamini uraia na tunu za taifa;
(c) Kuonesha kujiamini katika kujifunza nyanja mbalimbali zikiwemo sayansi na teknolojia, maarifa ya kinadharia na kivitendo;
(d) Kutumia stadi za lugha ikiwemo Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT), lugha mguso, lugha ya Kiswahili, Kiingereza na angalau lugha moja nyingine ya kigeni kuwasiliana;
(e) Kutumia maarifa ya masuala mtambuka kuyamudu mazingira yanayomzunguka; na
(f) Kutumia ujuzi na stadi kumwezesha mwanafunzi kujiajiri, kuajiriwa na kuyamudu maisha na mazingira yanayomzunguka.

## 5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Umahiri mkuu na umahiri mahususi unaotarajiwa kujengwa Kidato cha III–IV umebainishwa katika Jedwali Na.1.

**Jedwali Na. 1:** *Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Kidato cha III–IV*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kuthamini kazi za fasihi ya Kiswahili | 1.1 Kuonesha uelewa wa kazi za fasihi ya Kiswahili ya kitaifa<br>1.2 Kuhakiki kazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili |
| 2.0 Kujenga ujumi kutokana na kazi za fasihi | 2.1 Kujenga ujumi na falsafa ya Kiafrika katika kazi za fasihi<br>2.2 Kutumia kazi za fasihi katika kujenga hoja zenye mantiki |
| 3.0 Kubuni kazi za fasihi | 3.1 Kutathmini mbinu za kisanaa za utunzi wa kazi za kifasihi<br>3.2 Kutunga kazi sahili za kifasihi<br>3.3 Kutambua fursa zinazotokana na fasihi ya Kiswahili |

## 6.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji unategemea ushirikiano madhubuti baina ya mwalimu, mwanafunzi, na mzazi/mlezi. Majukumu yao ni kama yafuatayo:

### 6.1 Mwalimu

Mwalimu anatarajiwa:

(a) Kumwezesha mwanafunzi kujifunza na kupata umahiri uliokusudiwa katika somo la Fasihi ya Kiswahili;

(b) Kutumia mbinu za kufundishia na kujifunzia kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai, na uwezo wa mwanafunzi ili kumwezesha:

- (i) Kujenga umahiri unaohitajika katika Karne ya 21; na
- (ii) Kushiriki kikamilifu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

(c) Kutumia mbinu shirikishi zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji zikiwemo zile zinazomwezesha mwanafunzi kufikiri, kutafakari na kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali. Mbinu za kufundishia na kujifunzia zinazopendekezwa ni pamoja na; kazi za vitendo, utafiti, majadiliano na kazimradi zinazolenga kutatua matatizo halisi katika mazingira ya mwanafunzi. Aidha, mwalimu anahimizwa kutumia mbinu nyingine kama hizo kulingana na muktadha ili kufanikisha ujenzi wa umahiri uliokusudiwa;

(d) Kuandaa darasa salama lenye mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia;

(e) Kutengeneza au kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia;

(f) Kufanya upimaji endelevu mara kwa mara kwa kutumia zana na mbinu za upimaji na tathmini zinazopima nadharia na vitendo zikiwemo bunguabongo, orodhahakiki, majaribio, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi na kazi za vikundi), kazimradi na mkoba wa kazi. Zana na mbinu nyingine ni majaribio kwa vitendo, uwasilishaji, mitihani ya muhula na mtihani wa mwisho;



FASIHI YA KISWAHILISEKONDARI KIDATO CHA III-IV.indd 4 08/08/2023 15:07

(g) Kuhakikisha kuwa ufundishaji na ujifunzaji unafanyika kwa haki na usawa kwa kila mwanafunzi bila kujali tofauti zao;
(h) Kumlinda mwanafunzi awapo shuleni;
(i) Kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi ya kila siku;
(j) Kubaini mahitaji ya mwanafunzi na kutoa afua stahiki;
(k) Kushirikisha wazazi/walezi na jamii katika hatua mbalimbali za ujifunzaji wa mwanafunzi; na
(l) Kuchopeka masuala mtambuka na TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

### 6.2 Mwanafunzi

Mwanafunzi anatarajiwa:

(a) Kuwa mtendaji mkuu katika mchakato wote wa ujifunzaji;
(b) Kushiriki katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji ndani na nje ya darasa ili kupata umahiri unaokusudiwa; na
(c) Kushiriki katika kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali vikiwemo vitabu vya kiada, ziada na machapisho mengine kutoka katika maktabamtandao.

### 6.3 Mzazi/Mlezi

Mzazi/Mlezi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia maendeleo ya mtoto katika ujifunzaji;
(b) Kumsimamia mtoto kutekeleza kazi zake za kitaaluma pale inapowezekana;
(c) Kuhakikisha kuwa mazingira ya nyumbani ni rafiki na salama yanayowezesha ujifunzaji;
(d) Kufuatilia mwenendo wa tabia ya mtoto;
(e) Kumpatia mtoto vifaa vyote vinavyohitajika katika ujifunzaji;
(f) Kuhakikisha mtoto anapata mahitaji muhimu; na
(g) Kumfundisha mtoto umuhimu na thamani ya elimu na kazi pamoja na kumhimiza kujifunza kwa bidii.



FASIHI YA KISWAHILISEKONDARI KIDATO CHA III-IV.indd 5 08/08/2023 15:07

## 7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji ni msingi katika kujenga umahiri kwa mwanafunzi. Muhtasari huu umependekeza mbinu za ufundishaji na ujifunzaji kwa kila shughuli. Miongoni mwa mbinu hizo ni uchunguzi, kisamafunzo, majadiliano, maigizo, matembezi msambao, ziara za kimasomo, kazi za vitendo, na kazimradi. Hata hivyo, mwalimu anashauriwa kutumia mbinu nyingine kama hizo kulingana na muktadha wa ufundishaji na ujifunzaji.

## 8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unahitaji zana mbalimbali ili kujenga umahiri uliokusudiwa. Hivyo, mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kushirikiana katika kuandaa au kufaragua zana mbadala zinazopatikana katika mazingira ya shuleni na nyumbani pindi zinapohitajika. Mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kutafuta taarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ili kuleta ufanisi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa kutumika kwa ajili ya rejea vitatolewa na TET.

## 9.0 Upimaji

Upimaji ni mchakato muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Fasihi ya Kiswahili. Mwalimu anashauriwa kuwa na uwanja mpana wa uchaguzi wa mbinu na zana za upimaji wa Fasihi ya Kiswahili ili kupima uwezo wa mwanafunzi katika kuthamini kazi za fasihi ya Kiswahili, kujenga ujumi na falsafa ya Kiafrika katika kazi za fasihi na kubuni kazi za fasihi. Aidha, upimaji utajumuisha upimaji endelevu na upimaji tamati. Upimaji endelevu utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji na utamwezesha mwalimu kubaini uwezo na uhitaji wa mwanafunzi katika ujifunzaji. Zana za upimaji zinazoweza kutumika katika ufundishaji na ujifunzaji ni orodhahakiki, mazoezi ya darasani, majaribio, majaribio kwa vitendo, dodoso, maswali ya ana kwa ana, kazi kwa vitendo, kazi binafsi na kazi za vikundi, kazimradi na mkoba wa kazi na zana nyingine kama hizo. Hivyo, upimaji endelevu utachangia asilimia 30 ya upimaji wote na upimaji tamati wa kuhitimu Kidato cha Nne utachangia asilimia 70. Mgawanyo wa alama za upimaji endelevu na tamati umebainishwa katika Jedwali Na. 2.



FASIHI YA KISWAHILISEKONDARI KIDATO CHA III-IV.indd 6 08/08/2023 15:07

**Jedwali Na. 2**: *Mgawanyo wa Alama za Upimaji Endelevu na Tamati*

| Na. | Upimaji | Alama (%) |
|---|---|---|
| | Mtihani wa muhula wa kwanza Kidato cha III | 5 |
| | Mtihani wa muhula wa pili Kidato cha III | 5 |
| | Kazimradi | 5 |
| | Mtihani wa muhula wa kwanza Kidato cha IV | 5 |
| | Mtihani wa utamilifu wa Kidato cha IV | 10 |
| | Mtihani wa Taifa wa Kidato cha IV | 70 |
| **Jumla** | | **100** |

## 10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa Fasihi ya Kiswahili Elimu ya Sekondari Kidato cha III–IV unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za ujifunzaji. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi, ambapo kila kipindi ni dakika 40. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni viwili (2) kwa wiki.

## 11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Maudhui ya ufundishaji na ujifunzaji yamepangiliwa katika jedwali lenye vipengele saba ambavyo ni umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa, vigezo vya upimaji, zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa na idadi ya vipindi. Maudhui hayo yameoneshwa katika Jedwali Na. 3 na Na. 4.

## Kidato cha III

**Jedwali Na. 3:** *Maudhui ya Kidato cha III*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kuthamini kazi za fasihi ya Kiswahili | 1.1 Kuonesha uelewa wa kazi za fasihi ya Kiswahili ya kitaifa | (a) Kufafanua dhana ya fasihi ya Kiswahili ya kitaifa | **Uchunguzi**: Waongoze wanafunzi kuchunguza vitu vinavyopatikana katika mazingira yao (mavazi, nyimbo za kitaifa, misuko, vinyago, matini za kifasihi, michezo ya watoto), kisha wabainishe sifa za kitaifa kulingana na sanaa na vitu walivyochunguza<br>**Majadiliano**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili maana na sifa za fasihi ya Kiswahili ya kitaifa kutokana na sifa za sanaa na vitu walivyochunguza | Dhana ya fasihi ya Kiswahili ya kitaifa imefafanuliwa | Matini ya "wimbo wa Taifa, wimbo wa Tanzania, Tanzania, wimbo wa "Tazama Ramani," na wimbo wa "Mashujaa wa Zanzibar", matini za hadithi, ngano, mashairi ya kimapokeo na ya kisasa na matini za fasihi ya watoto | 8 |



FASIHI YA KISWAHILISEKONDARI KIDATO CHA III-IV.indd 8 08/08/2023 15:07

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Matembezi msambao**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili umuhimu wa fasihi ya kitaifa na kubandika kazi zao darasani, kisha wazitembelee na kuzisoma | | | |
| | | (b) Kuchambua sifa za fasihi ya Kiswahili ya kitaifa kwenye 'Wimbo wa Taifa', wimbo wa 'Tanzania Tanzania', wimbo wa 'Tazama Ramani' na wimbo wa 'Mashujaa wa Zanzibar' | **Nyimbo**:Waongoze wanafunzi kuimba 'Wimbo wa Taifa', wimbo wa 'Tanzania Tanzania', wimbo wa 'Tazama Ramani' na wimbo wa 'Mashujaa wa Zanzibar', kisha wachambue sifa za fasihi ya Kiswahili ya kitaifa kwenye nyimbo hizo | Sifa za fasihi ya Kiswahili ya kitaifa kwenye 'Wimbo wa Taifa', wimbo wa 'Tanzania Tanzania', wimbo wa 'Tazama Ramani' na wimbo wa Mashujaa wa Zanzibar zimechambuliwa | | |



FASIHI YA KISWAHILISEKONDARI KIDATO CHA III-IV.indd 9 08/08/2023 15:07

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kujadili sifa za fasihi ya kitaifa kwenye fasihi ya watoto | **Uchunguzi:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchunguza hadithi za watoto, kisha wajadili sifa za hadithi hizo<br>**Uchambuzi wa matini**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchambua matini za fasihi ya watoto, kisha wajadili sifa za fasihi ya kitaifa | Sifa za fasihi ya kitaifa kwenye fasihi ya watoto zimejadiliwa | | |
| | | (d) Kubainisha sifa za fasihi ya kitaifa kwenye ngano | **Masimulizi**:Wasimulie wanafunzi ngano au wasikilize ngano kwa kutumia vifaa vya TEHAMA, kisha waongoze kubainisha sifa za ngano uliyowasimulia au waliyoisikiliza<br>**Uchambuzi wa matini**:<br>Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchambua matini za ngano, kisha wabainishe sifa za fasihi ya kitaifa | Sifa za fasihi ya kitaifa kwenye ngano zimebainishwa | | |



FASIHI YA KISWAHILISEKONDARI KIDATO CHA III-IV.indd 10 08/08/2023 15:07

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) Kutunga shairi lenye sifa za fasihi ya kitaifa | **Bunguabongo**: Waongoze wanafunzi kubungua bongo kuhusu maana na sifa za shairi<br>**Uchunguzi:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchunguza matini za mashairi ya kimapokeo na ya kisasa, kisha wabainishe sifa za fasihi ya kitaifa kwenye mashairi hayo<br>**Fikiri-andika-jozisha-shirikisha:** Waongoze wanafunzi kutunga shairi la kimapokeo na la kisasa lenye sifa za fasihi ya kitaifa, kisha washirikishane mashairi waliyoyatunga na kubainisha sifa za fasihi ya kitaifa | Shairi lenye sifa za fasihi ya kitaifa limetungwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1.2 Kuhakiki kazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili | (a) Kuhakiki fani na maudhui katika kazi za fasihi ya watoto | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuhusianisha fani na maudhui katika kazi za fasihi<br>**Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili vipengele vya fani na maudhui katika matini za fasihi ya watoto<br>**Maswali na majibu:** Waulize wanafunzi maswali kuhusu nyimbo na maigizo yanayofanywa na watoto katika mazingira yao, kisha wajibu maswali hayo<br>**Matembezi msambao:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchambua vipengele vya fani na maudhui katika nyimbo na maigizo ya watoto na kubandika | Fani na maudhui katika kazi za fasihi ya watoto yamehakikiwa | Matini za fasihi ya watoto, filamu ya Kiswahili, vifaa vya kuigizia, video za fasihi ya watoto, vitabu teule vya fasihi ya watoto na video za vichekesho | 12 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | darasani, kisha kila kikundi kitembelee kila kazi na kuisoma<br>**Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kusoma vitabu vya fasihi ya watoto, kisha wahakiki fani na maudhui | | | |
| | | (b) Kuhakiki fani na maudhui ya kifasihi katika filamu za Kiswahili | **Igizodhima**: Waongoze wanafunzi kuigiza matukio yanayotokea katika jamii yao, kisha wahakiki vipengele vya fani na maudhui vilivyojitokeza katika igizo hilo<br>**Uchunguzi**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchunguza filamu moja ya Kiswahili kwa kutumia vifaa vya TEHAMA, kisha wahakiki vipengele vya fani na maudhui vilivyojitokeza | Fani na maudhui ya kifasihi katika filamu za Kiswahili yamehakikiwa | | |



FASIHI YA KISWAHILISEKONDARI KIDATO CHA III-IV.indd 13 08/08/2023 15:07

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kuhakiki fani na maudhui katika vichekesho | **Maigizo**: Wanafunzi wakiwa katika vikundi wapewe dhima za kuigiza vichekesho kuhusu masuala mtambuka, kisha wahakiki fani na maudhui katika vichekesho hivyo<br>**Majadiliano**: Waongoze wanafunzi kuangalia kichekesho kimoja kwa kutumia vifaa vya TEHAMA, kisha wahakiki fani na maudhui ya kichekesho hicho | Fani na maudhui katika vichekesho yamehakikiwa | | |
| 2.0 Kujenga ujumi kutokana na kazi za fasihi | 2.1 Kujenga ujumi na falsafa ya Kiafrika katika kazi za fasihi | (a) Kufafanua dhana na vipengele vya ujumi na falsafa ya Kiafrika katika fasihi | **Bunguabongo**: Waongoze wanafunzi kubungua bongo kuhusu maana na vipengele vya ujumi na falsafa ya Kiafrika katika fasihi | Dhana na vipengele vya ujumi na falsafa ya Kiafrika katika fasihi vimefafanuliwa | Matini zenye ujumi na falsafa ya Kiafrika, nyimbo zenye ujumi na falsafa ya Kiafrika na vitabu teule vya tamthiliya zenye ujumi na falsafa ya Kiafrika | 14 |



FASIHI YA KISWAHILISEKONDARI KIDATO CHA III-IV.indd 14 08/08/2023 15:07

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini zenye ujumi na falsafa ya Kiafrika, kisha wafafanue vipengele vya ujumi na falsafa ya Kiafrika vilivyojitokeza katika matini hizo<br>**Masimulizi ya hadithi**: Wasimulie wanafunzi hadithi yenye ujumi na falsafa ya Kiafrika, kisha wabainishe vipengele vya ujumi na falsafa ya Kiafrika katika hadithi hiyo<br>**Kazimradi:** Waongoze wanafunzi kukusanya hadithi zenye ujumi na falsafa ya Kiafrika katika jamii zao, kisha wachambue vipengele vya ujumi na falsafa ya | | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kiafrika katika hadithi hizo | | | |
| | | (b) Kubainisha ujumi na falsafa ya Kiafrika katika methali za Kiswahili | **Kisamafunzo**: Wasimulie wanafunzi kisamafunzo chenye methali mbalimbali, kisha wabainishe ujumi na falsafa ya Kiafrika katika methali hizo<br>**Mchezo**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kucheza mchezo wa methali. Mwanafunzi ataje methali yenye ujumi na falsafa ya Kiafrika na wengine wabainishe ujumi na falsafa ya Kiafrika katika methali hiyo | Ujumi na falsafa ya Kiafrika katika methali za Kiswahili imebainishwa | | |
| | | (c) Kuhakiki tamthiliya zenye ujumi na falsafa ya Kiafrika | **Uchambuzi wa matini**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kuhakiki ujumi na falsafa ya Kiafrika katika tamthiliya | Tamthiliya zenye ujumi na falsafa ya Kiafrika zimehakikiwa | | |



FASIHI YA KISWAHILISEKONDARI KIDATO CHA III-IV.indd 16 08/08/2023 15:07

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2.2 Kutumia kazi za fasihi katika kujenga hoja zenye mantiki | (a)Kuchanganua mambo ya kuzingatia wakati wa kujenga hoja kimantiki kutokana na kazi za fasihi | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchambua hoja zenye mantiki katika matini za kifasihi, kisha wachanganue mambo yaliyozingatiwa katika kujenga hoja hizo<br>**Utambaji wa ngonjera:** Waongoze wanafunzi kutazama na kusikiliza ngonjera iliyotambwa kwa kutumia vifaa vya TEHAMA, kisha wachanganue mambo yaliyozingatiwa wakati wa kujenga hoja zenye mantiki katika utambaji wa ngonjera | Mambo ya kuzingatia wakati wa kujenga hoja kimantiki kutokana na kazi za fasihi yamechanganuliwa | Chati ya kielelezo cha ujenzi wa hoja za kimantiki, matini za kifasihi, insha za kisanaa, video ya utambaji wa ngonjera na video ya mdahalo wa kifasihi | 10 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kuandika insha za kisanaa zenye hoja za kimantiki | **Uchunguzi**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchunguza insha za kisanaa zenye hoja za kimantiki, kisha wabainishe sifa za insha hizo<br>**Mlolongo wa matukio**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kuandaa mlolongo wa matukio wanayoyafahamu, kisha waandike insha ya kisanaa yenye hoja zenye mantiki kwa kurejelea matukio hayo | Insha za kisanaa zenye hoja za kimantiki zimeandikwa | | |
| | | (c) Kutumia fasihi kuwasilisha hoja kimantiki katika midahalo | **Uchunguzi**: Waongoze wanafunzi kuangalia mdahalo wa kifasihi kwa kutumia vifaa vya TEHAMA, kisha wachunguze namna hoja zinavyowasilishwa katika mdahalo huo | Fasihi imetumiwa kuwasilisha hoja kimantiki katika midahalo | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Mdahalo**: Waongoze wanafunzi kufanya mdahalo wa kifasihi, kisha wajadili hoja zenye mantiki zilizojitokeza katika mdahalo huo | | | |
| 3.0 Kubuni kazi za fasihi | 3.1 Kutathmini mbinu za kisanaa za utunzi wa kazi za kifasihi | (a) Kufafanua mbinu za kisanaa katika utungaji wa kazi za kifasihi | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kusikiliza nyimbo zilizorekodiwa, kisha katika vikundi wafafanue mbinu za kisanaa zilizotumika katika nyimbo hizo<br>**Uchambuzi wa matini**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchambua matini za hadithi fupi na mashairi, kisha wafafanue mbinu za kisanaa zilizotumika katika hadithi na mashairi hayo | Mbinu za kisanaa katika utungaji wa kazi za kifasihi zimefafanuliwa | Nyimbo zilizorekodiwa, matini za hadithi fupi, mashairi na ngano | 12 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Kumwalika mgeni:** Mwalike mtunzi wa kazi za fasihi, kisha waongoze wanafunzi wamuulize maswali kuhusu mbinu za kisanaa alizozitumia katika kazi zake. Ikiwezekana, akaribishwe mtunzi ambaye wanafunzi wamesoma kazi yake | | | |
| | | (b) Kulinganisha matumizi ya mbinu za kisanaa katika kazi mbalimbali za kifasihi | **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kulinganisha matumizi ya mbinu za kisanaa katika hadithi na mashairi, kisha wajadiliane kwa pamoja | Matumizi ya mbinu za kisanaa katika kazi za kifasihi yamelinganishwa | | |
| | | (c) Kujadili mbinu za kisanaa katika ngano | **Uchambuzi wa matini**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchambua ngano mbalimbali, kisha wajadili mbinu za kisanaa zilizotumika katika ngano hizo | Mbinu za kisanaa katika ngano zimejadiliwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 3.2 Kutunga kazi sahili za kifasihi | (a) Kufafanua kanuni za utunzi wa mashairi | **Matembezi msambao**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kufafanua kanuni za utunzi wa mashairi ya kimapokeo na kisasa, kisha wazibandike darasani, wazitembelee na kuzisoma | Kanuni za utunzi wa mashairi zimefafanuliwa | Matini za mashairi ya kimapokeo na kisasa, matini za kazi za fasihi ya watoto na nyimbo zilizorekodiwa | 14 |
| | | (b) Kutunga mashairi sahili | **Oneshombinu**: Waoneshe wanafunzi namna ya kughani mashairi ya kimapokeo na kisasa, kisha waghani mashairi hayo na kubainisha mawazo makuu yaliyomo katika mashairi hayo<br>**Fikiri-andika**: Waongoze wanafunzi kutunga mashairi sahili ya kimapokeo na kisasa, kisha wayaghani | Mashairi sahili yametungwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kufafanua kanuni za utunzi wa kazi za fasihi ya watoto | **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kufafanua kanuni za utunzi wa kazi za fasihi ya watoto, kisha wajadiliane kwa pamoja | Kanuni za utunzi wa kazi za fasihi ya watoto zimefafanuliwa | | |
| | | (d) Kutunga kazi sahili za fasihi ya watoto | **Mfululizo wa matukio**: Wape wanafunzi matukio mbalimbali yenye mfuatano, kisha watunge hadithi sahili za watoto kwa mfuatano wa matukio hayo<br><br>**Fikiri-andika**: Waongoze wanafunzi kubuni kisa cha watoto, kisha watunge hadithi sahili ya watoto | Kazi sahili za fasihi ya watoto zimetungwa | | |

## Kidato cha IV

**Jedwali Na. 4:** *Maudhui ya Kidato cha IV*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kuthamini kazi za fasihi ya Kiswahili | 1.1 Kuhakiki kazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili | (a) Kuhakiki fani na maudhui katika nyimbo za zamani (kabla ya mwaka 1990) na za kisasa (baada ya mwaka 1990) | **Nyimbo**: Waongoze wanafunzi kusikiliza nyimbo za zamani (kabla ya mwaka 1990) kwa kutumia vifaa vya TEHAMA, kisha wahakiki fani na maudhui ya nyimbo hizo<br>**Uchambuzi wa matini**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kusoma matini za nyimbo za kisasa (baada ya mwaka 1990), kisha wahakiki vipengele vya fani na maudhui<br><br>**Kazimradi**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kutafuta nyimbo za kisasa | Fani na maudhui katika nyimbo za zamani (kabla ya mwaka 1990) na za kisasa (baada ya mwaka 1990) yamehakikiwa | Nyimbo za zamani zilizorekodiwa (kabla ya mwaka 1990) na za kisasa ( baada ya mwaka 1990), nyimbo za taarabu za zamani zilizorekodiwa (kabla ya mwaka 1990) na za kisasa (baada ya mwaka 1990) na filamu zilizotafsiriwa kwa Kiswahili | 16 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | (baada ya mwaka 1990), kisha wahakiki fani na maudhui katika nyimbo hizo | | | |
| | | (b) Kuhakiki fani na maudhui katika nyimbo za taarabu za zamani (kabla ya mwaka 1990) na za kisasa (baada ya mwaka 1990) | **Bunguabongo**: Waongoze wanafunzi kubungua bongo kwa kubainisha nyimbo za taarabu za zamani (kabla ya mwaka 1990) na za kisasa (baada ya mwaka 1990)<br>**Majadiliano**: Waongoze wanafunzi kutazama na kusikiliza wimbo wa taarabu wa zamani (kabla ya mwaka 1990) kwa kutumia vifaa vya TEHAMA, kisha katika vikundi wahakiki vipengele vya fani na maudhui katika wimbo huo<br>**Nyimbo**: Waongoze wanafunzi kuimba wimbo wa taarabu wa kisasa (baada ya mwaka 1990), | | | |



FASIHI YA KISWAHILISEKONDARI KIDATO CHA III-IV.indd 24 08/08/2023 15:07

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | kisha wahakiki fani na maudhui ya wimbo huo<br>**Uchambuzi wa matini**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kusoma matini ya nyimbo za taarabu za zamani (kabla ya mwaka 1990), kisha wahakiki fani na maudhui | | | |
| | | (c) Kuhakiki fani na maudhui ya kifasihi katika filamu zilizotafsiriwa | **Igizodhima**: Waongoze wanafunzi kuigiza tukio lolote katika jamii, kisha wahakiki fani na maudhui ya igizo hilo<br>**Majadiliano**: Waongoze wanafunzi kuangalia filamu iliyotafsiriwa kwa Kiswahili, kisha katika vikundi wahakiki fani na maudhui ya filamu hiyo | Fani na maudhui ya kifasihi katika filamu zilizotafsiriwa yamehakikiwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kujenga ujumi kutokana na kazi za fasihi | 2.1 Kujenga ujumi na falsafa ya Kiafrika katika kazi za fasihi | (a) Kuhakiki riwaya zenye ujumi na falsafa ya Kiafrika | **Uchambuzi wa matini**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kuhakiki riwaya zenye ujumi na falsafa ya Kiafrika | Riwaya zenye ujumi na falsafa ya Kiafrika zimehakikiwa | Matini zenye ujumi na falsafa ya Kiafrika, nyimbo za Kiswahili zenye ujumi na falsafa ya Kiafrika, vitabu teule vya riwaya zenye ujumi na falsafa ya Kiafrika na ngano zenye ujumi na falsafa ya Kiafrika | 14 |
| | | (b) Kuhakiki ngano zenye ujumi na falsafa ya Kiafrika | **Uchambuzi wa matini**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kuhakiki ujumi na falsafa ya Kiafrika katika ngano mbalimbali<br>**Kazimradi**: Waongoze wanafunzi kutafuta ngano katika jamii zao, kisha wachambue ujumi na falsafa ya Kiafrika katika ngano hizo | Ngano zenye ujumi na falsafa ya Kiafrika zimehakikiwa | | |
| | | (c) Kuhakiki nyimbo za Kiswahili zenye ujumi na falsafa ya Kiafrika | **Nyimbo**: Waongoze wanafunzi kuimba nyimbo za Kiswahili wanazozifahamu, kisha wahakiki ujumi na falsafa ya Kiafrika katika nyimbo hizo | Nyimbo za Kiswahili zenye ujumi na falsafa ya Kiafrika zimehakikiwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Kazimradi**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kukusanya nyimbo za Kiswahili, kisha wahakiki ujumi na falsafa ya Kiafrika | | | |
| | | (d) Kujadili nafasi ya ujumi na falsafa ya Kiafrika katika jamii | **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili nafasi ya ujumi na falsafa ya Kiafrika katika jamii | Nafasi ya ujumi na falsafa ya Kiafrika katika jamii imejadiliwa | | |
| | 2.2 Kutumia kazi za fasihi katika kujenga hoja zenye mantiki | (a) Kutumia riwaya kuandika hotuba zenye hoja za kimantiki | **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili namna riwaya zinavyoweza kutumika kuandika hotuba zenye hoja za kimantiki<br>**Fikiri-andika-shirikisha**: Waongoze wanafunzi kufikiria mada wanayoipenda, kisha watumie maarifa na stadi za riwaya kuandika hotuba yenye hoja za kimantiki | Riwaya zimetumiwa katika kuandika hotuba zenye hoja za kimantiki | Vitabu teule vya riwaya, mwongozo wa maswali ya usaili, usaili uliorekodiwa/ video ya usaili na magazeti yenye maudhui ya usaili | 12 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kutumia maigizo kujenga hoja kimantiki katika usaili | **Bunguabongo**: Waongoze wanafunzi kubungua bongo kuhusu maana, sifa na mambo ya kuzingatia wakati wa usaili<br>**Majadiliano**: Waongoze wanafunzi kuangalia namna usaili unavyofanyika kwa kutumia vifaa vya TEHAMA, kisha katika vikundi wajadili namna hoja za kimantiki zilivyojengwa katika usaili huo<br>**Igizodhima**: Andaa mwongozo wa usaili, kisha wanafunzi wautumie katika igizo la usaili kwa kujenga hoja kimantiki | Maigizo yametumiwa kujenga hoja kimantiki katika usaili | | |



FASIHI YA KISWAHILISEKONDARI KIDATO CHA III-IV.indd 28 08/08/2023 15:07

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kutumia ngonjera kujenga hoja kimantiki katika mawasiliano ya kitaaluma | **Kutamba ngonjera**: Waongoze wanafunzi kutamba ngonjera, kisha waeleze namna walivyojenga hoja kimantiki kwenye ngonjera hiyo<br>**Mdahalo**:Waongoze wanafunzi kutumia stadi za ngonjera kufanya mdahalo kwa kujenga hoja kimantiki katika mawasiliano ya kitaaluma | Ngonjera zimetumiwa kujenga hoja kimantiki katika mawasiliano ya kitaaluma | | |
| 3.0 Kubuni kazi za fasihi | 3.1 Kutunga kazi sahili za kifasihi | (a) Kuchambua kanuni za utunzi wa tamthiliya | **Uchambuzi wa matini**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchambua kanuni za utunzi wa tamthiliya | Kanuni za utunzi wa tamthiliya zimechambuliwa | Matini za tamthiliya, riwaya na hadithi, na video za vichekesho | 12 |
| | | (b) Kutunga tamthiliya fupi | **Kisa/tukio:** Wasimulie wanafunzi kisa/tukio kwa ufupi kwa mtindo wa mazungumzo, kisha wanafunzi waendeleze kisa hicho kwa mtindo huo wa mazungumzo | Tamthiliya fupi zimetungwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Ziara**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kutembelea sehemu mbalimbali (sokoni, vituo vya mabasi, hospitalini, gulioni) na kuandika matukio watakayoyaona, kisha watunge tamthiliya fupi kuhusu matukio hayo<br>**Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kwa kutumia maswali na majibu kubuni visa na matukio mbalimbali, kisha watunge tamthiliya fupi | | | |
| | | (c) Kuchambua kanuni za utunzi wa riwaya | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchambua kanuni za utunzi wa riwaya | Kanuni za utunzi wa riwaya zimechambuliwa | | |
| | | (d) Kutunga riwaya sahili | **Ukamilishaji wa hadithi:** Wape wanafunzi sehemu fupi ya hadithi kuhusu tukio lolote, kisha | Riwaya sahili zimetungwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | waendeleze tukio hilo kwa kuandika riwaya sahili yenye uchangamani wa visa na matukio<br><br>**Fikiri-andika**:<br>Waongoze wanafunzi kubuni wahusika, visa na matukio changamani, kisha waandike riwaya sahili | | | |
| | | (e) Kuchambua kanuni za utunzi wa vichekesho | **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi kuangalia vichekesho kwa kutumia vifaa vya TEHAMA, kisha katika vikundi wachambue kanuni za utunzi wa vichekesho kutokana na vichekesho hivyo | Kanuni za utunzi wa vichekesho zimechambuliwa | | |
| | | (f) Kutunga vichekesho | **Fikiri-andika-jozisha-shirikisha**: Waongoze wanafunzi kufikiria matukio yanayotokea katika jamii, kisha | Vichekesho vimetungwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | watunge vichekesho kuhusiana na matukio hayo | | | |
| | 3.2 Kutambua fursa zinazotokana na fasihi ya Kiswahili | (a) Kubaini fursa za utunzi wa kazi za kifasihi | **Bunguabongo**: Waongoze wanafunzi kubungua bongo kuhusu fursa zinazotokana na utunzi wa kazi za kifasihi | Fursa za utunzi wa kazi za kifasihi zimebainishwa | Machapisho mbalimbali ya kifasihi, filamu za kazi za kifasihi, vitabu teule vya fasihi ya watoto na kazi za kifasihi zinazopatikana katika mitandao ya kijamii | 16 |
| | | (b) Kuchambua fursa za kutafsiri na kuhariri kazi za kifasihi | **Kumwalika mgeni:** Mwalike mgeni mwenye ujuzi wa kutafsiri na kuhariri kazi za kifasihi ili ajadiliane na wanafunzi kuhusu kutafsiri na kuhariri kazi za kifasihi, pamoja na fursa zake<br>**Matembezi msambao**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kuandika fursa za kutafsiri na kuhariri kazi za kifasihi walizojadili na mgeni | Fursa za kutafsiri na kuhariri kazi za kifasihi zimechambuliwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kuchambua fursa za kuandaa filamu zinazotokana na kazi za kifasihi | **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili fursa za kuandaa filamu zinazotokana na kazi za kifasihi | Fursa za kuandaa filamu zinazotokana na kazi za kifasihi zimefafanuliwa | | |
| | | (d) Kuchambua fursa za uandishi wa vitabu vya fasihi ya watoto | **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchambua fursa za uandishi wa vitabu vya fasihi ya watoto | Fursa za uandishi wa vitabu vya fasihi ya watoto zimechambuliwa | | |
| | | (e) Kuchambua fursa za uchapishaji wa kazi za fasihi | **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchambua fursa za uchapishaji wa kazi za fasihi<br>**Kumwalika mgeni**: Mwalike mgeni aliyechapicha kazi za fasihi ili ajadiliane na wanafunzi kuhusu fursa mbalimbali zinazotokana na kazi alizochapisha | Fursa za uchapishaji wa kazi za fasihi zimechambuliwa | | |



FASIHI YA KISWAHILISEKONDARI KIDATO CHA III-IV.indd 33 08/08/2023 15:07

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (f) Kuhusianisha fursa za kazi za kifasihi na TEHAMA | **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi katika vikundi kuhusianisha fursa za kazi za kifasihi na TEHAMA katika maisha yao ya kila siku<br><br>**Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili namna ya kutumia nyenzo na majukwaa ya ki-TEHAMA kama vile mitandao ya kijamii kwa ajili ya kutangaza na kuuza kazi za kifasihi<br><br>**Kumwalika mgeni**: Mwalike mgeni mwenye ujuzi wa fasihi na TEHAMA ajadiliane na wanafunzi namna TEHAMA inavyoweza kutumika katika kupata fursa za kazi za kifasihi | Fursa za kifasihi na TEHAMA zimehusianishwa | | |

## Bibliografia


Abedi, K. A. (1954). *Sheria za kutunga mashairi na Diwani ya Amri.* East African Literature Bureau.

Bakize, L. H. (2014). *Utangulizi wa fasihi ya watoto.* Moccony Printing Press.

Kahigi, K. K. & Mulokozi, M. M. (1979). *Kunga za ushairi na diwani.* Tanzania Publishing House.

King'ei, K., & Kisovi, C. N. M. (2005). *Msingi wa fasihi simulizi*. Kenya Literature Bereau.

Madumulla, J. S. (2009). *RIWAYA YA KISWAHILI: Nadharia, historia na misingi ya uchambuzi*. Phoenix Publishers.

Msokile, M. (1993*). Misingi ya uhakiki*. Dar es Salaam University Press.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa fasihi ya Kiswahili*. Moccony Printis Press.

Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi*: *nadharia na mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation.

Samwel, M. (2013). *Ushairi wa Kiswahili: Nadharia, maendeleo, mwongozo kwa walimu wa Kiswahili na Diwani ya MEA*. Meveli Publishers.

Senkoro, F. E. M. K. (1987). *Fasihi na jamii*. Press and Publicity Centre.

Senkoro, F.E.M.K. (2011). *Fasihi*. KAUTTU Limited.

Taasisi ya Elimu Tanzania (1976). *Fasihi simulizi katika sekondari.* Dar es Salaam University Press.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa fasihi, misingi na vipengele vyake*. Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2008). *Misingi ya uchanganuzi wa fasihi.* Vide-Muwa Publishers Limited.




FASIHI YA KISWAHILISEKONDARI KIDATO CHA III-IV.indd 35 08/08/2023 15:07